


# HALMASHAURI YA MJI WA IFAKARA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji)



Simu: 023 - 2931523  
Fax: 023 - 2931513  
E-mail : [info@ifakaradc.go.tz](mailto:info@ifakaradc.go.tz)  
[www.ifakaradc.go.tz](http://www.ifakaradc.go.tz)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji,  
S. L P. 433,  
**IFAKARA**

## TAARIFA KWA UMMA.

### WANAFUNZI 2913 KUFANYA MITIHANI YA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI KATIKA HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.

Jumla ya Wanafunzi 2913 kati yao Wavulana wakiwa ni 1409 na Wasichana 1504 wanafanya Mitihani ya kumaliza elimu ya Msingi katika Halmashauri ya Mji Ifakara iliyoanza 06.09.2017 nchini kote na inayotarajiwa kumalizika 07.09.2017.

Mkuu wa Idara ya elimu msingi katika Halmashauri ya Mji Ifakara Bi. Mariamu Nnauye ameeleza kuwa Halmashauri ya Mji ilifanya usajili wa Watahiniwa wote kwenye mfumo wa Baraza la mitihani [PREM] kuanzia Januari 2017 kwa shule 38 kati ya shule 39. Hata hivyo alifafanua kuwa shule moja ya binafsi haina Watahiniwa wa darasa la VII kwa mwaka huu na hivyo kupelekea idadi hiyo ya Watahiniwa kwa shule 38 huku 33 zikiwa ni shule za Serikali na 6 zisizo za serikali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Ifakara Ndugu. Francis K. Ndulane amewataka heri Watahiniwa wote na amewataka kutambua kuwa hatua hiyo ni sehemu muhimu katika kufikia ndoto zao za maisha ya baadae hivyo wanapaswa kuwa makini na kufanya mitihani hiyo kwa weledi

Aidha Mkurugenzi amewataka wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia zoezi hilo la mitihani katika Halmashauri ya Mji Ifakara kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Sheria na Miongozo waliyopewa ili kufanikisha zoezi hilo bila dosari yeyote.

  
Fatna Mfalingundi,  
**AFISA HABARI,**

**HALMASHAURI YA MJI IFAKARA.**

**06.07.2017**